

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA THELATHINI NA TISA

30 JUNI, 2015



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA THELATHINI NA TISA – TAREHE 30 JUNI, 2015

I. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

279. MHESHIMIWA MOZA ABEDI SAIDY (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Katika Wilaya ya Kondoa Kata ya Pahi kuna Zahanati iliyojengwa na wananchi hadi kufikia lenta na sasa ni miaka kumi (10) bado haijakamilika na tuna fununu ya kuingizwa fedha zipatazo milioni 30 katika Akaunti ya Kijiji kwa ajili ya kumalizia jengo hilo lakini mpaka sasa hakuna kilichofanyika:-

Je, ni lini jengo hilo litamalizika ili Wananchi wapate huduma bora za afya katika zahanati hiyo.

**280. MHESHIMIWA DKT. MARY MACHUCHE
MWANJELWA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Kutokana na kodi/tozo kubwa wanayotozwa wafanyabiashara wa Jiji la Mbeya ambayo hailingani na mapato; kumekuwa na wimbi kubwa la wafanyabiashara hao kuhamia Dar es Salaam hali inayosababisha Jiji la Mbeya kudumaa:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweka *fixed rate* ya kodi/tozo hizo.

**281. MHESHIMIWA JOHN PAUL LWANJI
(MANYONI MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Serikali iliahidi kusogeza huduma zaidi kwa Wananchi wa Wilaya ya Manyoni kwa kuongeza Halmashauri nyingine na kuwa Halmashauri mbili:-

Je, ni lini mpango huo utatekelezwa.

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

282. MHESHIMIWA SUSAN ANSELM LYIMO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi:- Katika siku za karibuni baadhi ya Vytho Vikuu hapa nchini vimekuwa vikianzishwa bila kufuata utaratibu hali inayosababisha wanafunzi kufundishwa chini ya viwango:-

Je, Serikali inatoa tamko gani.

283. MHESHIMIWA CHRISTOWAJA GERSON MTINDA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi:- Ripoti ya CAG ya Mwaka 2009/2010 inaeleza kwamba kuanzia mwaka 1994 hadi Juni, 2009 Bodi ya Mikopo ya Vytho Vikuu ilikuwa imetoa shilingi Bilioni 433.3 kama mikopo na kati ya fedha hizo shilingi bilioni 80.9 ni mikopo inayotakiwa kurejeshwa; na kwa kuwa wanafunzi husika walishamaliza masomo:-

Je, mpaka sasa Bodi imeshakusanya kiasi gani cha fedha na bado inadai kiasi gani.

WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

284. MHESHIMIWA SULEIMAN NCHAMBI SULEIMAN (KISHAPU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:-

Je, kwa nini TANESCO wasilipe fidia kwa Wananchi wanapokata umeme ghafla na kusababisha hasara ya kuunguza vitu na hasara za kiuchumi.

285. MHESHIMIWA DKT. DALALY PETER KAFUMU (IGUNGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha Mradi wa kupeleka umeme katika Tarafa ya Igurubi, Kata za Itumba na Mbutu.

WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII:

286. MHESHIMIWA MUHAMMAD IBRAHIM SANYA (MJI MKONGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:- Dawa yoyote ni sumu katika mwili wa binadamu na dawa nyingine zina

nguvu zaidi kulingana na aina ya maradhi inayotibu; kwa watu waliopata maradhi ya UKIMWI wanatumia dawa kali hivyo wanahitaji lishe bora kukabiliana na ukali wa dawa hizo:-

Je, Serikali mbali na kutoa huduma ya dawa, inawalishaje wagonjwa hao kwa kuwapa lishe bora.

**287. MHESHIMIWA SABREENA HAMZA
SUNGURA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:- Serikali imekuwa ikifungia vituo vya watoto yatima kupitia Kamati za Wilaya za Usalama wa Mtoto kwa sababu vituo hivyo havikizi haja kwa Mujibu wa Sheria:-

Je, kwa nini Serikali isiviwezeshe vituo hivi badala ya kuvifungia ili viweze kuleta tija kwenye jamii.

**DODOMA
30 JUNI, 2015**

**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**